**Learning by Ear 2011 Biashara – Kuanzisha Biashara**
**Kipindi cha 1: "Motisha"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Characters:

SIMULIZI

Daniel Huba (MWANAMUME, UMRI WA MIAKA 29, MWINGEREZA)

## Scene 1:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

## Scene 2:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

## Scene 3:

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**Mrs. SAGONDA:** (Mwanamke, umri wa miaka 53)

**Mr. MASINGA:** (Mwanamume, umri wa miaka 57)

## INTRO

**Host:**

Hamjambo na karibuni kwenye mfululizo wetu mpya wa vipindi vya *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* vinavyohusu kuanzisha biashara. Katika vipindi kumi vitakavyofuata, tutatambua hatua kuu za kufuata mtu anapotaka kuanzisha biashara yake binafsi. Daniel Huba, mhadhiri wa Kituo cha Ustawi

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

wa Ujasiriamali katika Chuo Kikuu cha Inoorero, atatupa ushauri wa kina kuhusu mambo yanayotakikana kufanywa. Aidha, tutafuatilia kisa cha Abbas, Mariam na Kossi ambao wamemaliza masomo hivi karibuni na hawana budi kujitosa kwenye hali halisi ya maisha. Hiki ndicho kipindi chetu cha kwanza, kuhusu motisha.

## Scene 1: On the street

## ABBAS, MARIAM, KOSSI

| |
|---|
| **1. SFX : Atmo from outside, daytime. Traffic noise, motorbikes.** |

| | |
|---|---|
| **2. MARIAM:** | **(Arrives and is ecstatic**) Duh! Mambo si mabaya, wenzangu – Nimepita kwa alama ya juu zaidi! |
| **3. KOSSI:** | **(happy)** Kawaida, wala si ajabu. Hongera! Tusherehekee matokeo yako! |
| **4. ABBAS:** | **(In a killjoy manner)** Naam, lakini sijali sana matokeo, nafikiria mustakabali. Kupata ajira! |
| **5. MARIAM:** | **(Interrupts, reassuringly)** Usijali! Hatutakosa mbinu za kutafuta riziki. |
| **6. KOSSI:** | **(Replies, dryly)** Natumai hivyo! Hasa kwa kuwa sasa inatubidi kuwakimu wazazi wetu kifedha. |
| **7. MARIAM:** | **(Still enthusiastic)** Twendeni. Twendeni zetu tukapate kinywaji… tutayazungumzia haya huko. |
| **8. Narrator:** | Mambo si mazuri sana kwa marafiki hao watatu, ambao hawawezi tena kuendelea na masomo- kwa sasa. Kama mtakavyosikia, wako tayari kujiajiri wenyewe. Hata hivyo wanahitaji kujibidiisha, kama mtaalamu wetu Daniel Huba anavyosema. |

**9. Daniel Huba : 1'07"**

*Mwanzo unahitaji wazo. Sote tuna mawazo, malengo, tungependa kujiunga na shule au chuo kikuu fulani, au tukiwa wachanga tungetaka kujiundia kundi la uigizaji au mchezo fulani. Wazo ni muhimu mtu anapotaka kuanzisha biashara. Na ukiwa na wazo na ukaamua kulitekeleza basi hali hiyo inakupa motisha. Ni tofauti na kuajiriwa. Vizuri kuajiriwa, kwenda shule na kupata kazi hatimaye. Lakini hata walioajiriwa wanapaswa kujiuliza wanavyoweza kufanya ili wafanye kazi zao binafsi.*

*Hatua ya kwanza ni kuwa na wazo la biashara. Ni muhimu kutambua kwamba biashara si kwamba inaingiza sokoni bidhaa au huduma mpya tu bali pia inaweza kumpa mtu faida- muhimu sana kuelewa hivyo.*

**10. Narrator:** Kizingiti cha kwanza ni kupata wazo linalovutia zaidi litakalokufanya uwe na motisha kwa muda mrefu. Wenzetu wanaelewa hilo? Ebu tuungane nao mkahawani tuwasikie wanavyojadiliana.

**Scene 2: ABBAS, MARIAM, KOSSI**

| **11. SFX : Bar atmo. Background music. Traffic noise.** |
|---|

| **12. SFX: liquid being poured into glasses** |
|---|

**13. MARIAM:** **(Drinks and talks)** Naam! Ebu tujikumbusheni. Hatuna namna. Tumekuwa tukiyazungumza haya kwa zaidi ya saa moja, tunazunguka pale pale!

| | | |
|---|---|---|
| **14.** | **KOSSI:** | Haya! Ebu zingatieni…. Mashirika ya serikali na pia ya kibinafsi hayawaajiri watu kwa sababu ya matatizo ya kifedha yaliyopo… |
| **15.** | **ABBAS:** | Hata wengi wa wazee wetu hawana ajira! |
| **16.** | **MARIAM:** | Tunaweza kupeleka maombi ya kufanya mazoezi kwa malipo kwenye shirika la serikali! |
| **17.** | **ABBAS:** | **(Mocking)** Nisikilize mwenzangu, wenyewe wamekumbwa na matatizo ya kifedha pia, hakuna yeyote miongoni mwao aliye tayari tena kulipa wanaofanya mazoezi. **(to KOSSI)** Kakako anayajua haya, au siyo, Kossi? |
| **18.** | **KOSSI:** | Naam, Anajua! Amekuwa akifanya hayo mazoezi kwa miaka miwili bila kupata hata ndururu. Wazazi wetu humsaidia mara nyingine! |
| **19.** | **MARIAM:** | **(Suddenly)** Subiri! Na vipi kwenye nyanja ya taasisi za kutoa misaada? |
| **20.** | **ABBAS:** | Si rahisi kama unavyofikiri. Nyanja yenyewe tayari imejaa wala haifanyi kazi inavyopaswa. Tuna mamilioni ya mashirika yasiyo ya serikali na mashirika ya kutoa misaada. |
| **21.** | **KOSSI:** | Na yapo huku kwetu kufaidika kwa fedha za mataifa ya magharibi, jambo ambalo linaridhiwa kabisa na viongozi wa mashirika hayo. |
| **22.** | **MARIAM:** | **(Slightly annoyed)** Sawa! Sawa! Sawa! Nishafahamu. Lakini tufanye nini? Hatuwezi kukaa tu bila kufanya kitu. Tunahitaji kazi! |

| | | |
|---|---|---|
| **23.** | **KOSSI:** | Kazi, naam, lakini sasa hivi tunahitaji bia! **(He shouts to the waitress)** Chupa tatu za bia tafadhali. |
| **24.** | **ABBAS:** | **(Suddenly enthusiastic)** Jamaa, hatuna namna, basi mbona tusianzishe biashara yetu? |
| **25.** | **MARIAM:** | **(Surprised)** Una maana gani? |
| **26.** | **ABBAS:** | (**Convincingly**) Ushasikia. Tufanyeni hivyo, tuweni na ujasiri. Tunaweza kuanzisha kampuni yetu, biashara yetu wenyewe. Ikiwa hakuna namna nyingine, tunaweza kuanzisha biashara wenyewe. |
| **27.** | **KOSSI:** | Na hivyo pia si rahisi, rafiki yangu. Kwanza ni lazima uwe na wazo zuri, mpango mzuri, vinginevyo hiyo ni ndoto! Na unahitaji mtaji kufanya hivyo! |
| **28.** | **ABBAS:** | Aaah, usiwe mtu wa kutamauka. Utapoteza nini ukijaribu? |
| **29.** | **MARIAM:** | **(Happy again)** Sikizeni, si vigumu… Tunaweza kufungua baa kama hii kwa mfano… |
| **30.** | **KOSSI:** | **(Ironically)** Au tunaweza kufungua mahali papya pa kuandaa mazishi- ukizingatia vita vyote na njaa, watu wanakufa kwa wingi hapa! **(Silence)** Pffff, Sioni tukifaulu! |

**31.** **ABBAS** and **MARIAM:** **(In chorus)** Kwa nini tusifaulu!

| | | |
|---|---|---|
| **32.** | **Narrator:** | Wana mawazo tofauti. Je watakata tamaa mapema kabla ya kujaribu? Mtaalamu wetu Daniel anasema wanatakikana kujihimiza. |

**33.** **Daniel Huba: 30''**

*Mara nyingi mtu anapokuwa na wazo jipya au aamue kutenda jambo la kipekee, kuna watu wengi walio karibu naye wanaomtatiza. Ndiposa unahitaji*

*motisha kuendelea na mipango yako. Motisha inahusiana moja kwa moja na "mahaba". Wafanyi biashara hufaulu kwa sababu ya motisha yao, kwasababu ya mahaba yao kwa jambo wanalotaka kutenda. Ni hisia za ndani zinazowahimiza watu kuendeleza nia zao bila kujali fikira za wengine..*

**34. Narrator:** Ebu tusikie iwapo rafiki zetu wana shauku kutekeleza nia yao. Majuma mawili yamepita baada ya mijadala ya muda mrefu na wamekubaliana kushirikiana kuanzisha biashara, lakini hata hivyo hawajajua biashara gani ya kushughulikia. Fauka ya hayo, si kila mtu anayefikiria kuwa mipango yao ni wazo zuri.

## Scene 4 : At Mrs. SAGONDA's

**MARIAM, ABBAS, KOSSI, Mrs. SAGONDA, Mr. MASINGA**

**35. SFX : Inner courtyard, calm, birds in background**

**36. SFX : Sounds of table, cutlery, dishes, water being poured into glasses**

**37. KOSSI:** Asante, Bi. Sagonda, asante sana. Chakula kitamu sana. Laiti ungekuwa na binti mwingine! **(bursts out laughing)**

**38. Mrs. SAGONDA:** Nina binti mmoja, Mariam. Lakini unajua wanangu wa kiume vyema, au siyo? Mbona usiwapatie dada zako?! **(laughter)**

**39. MARIAM:** **(Embarrassed)** Ma!

**40. ABBAS and KOSSI: (In chorus)** Mbona? **(general hysterics)**

**41. MARIAM:** **(Peremptorily)** Haya basi, tuzungumzieni masuala muhimu. Msisahau mmekuja hapa tuzungumzie mambo tuliyojadiliana, mawazo ya mustakabali wetu, na kuamua uwanja gani tujihusishe nao.

**42. Mrs. SAGONDA:** (**With a reproachful tone**) Ati nini, bado unashikilia hilo wazo potovu la kuanzisha kazi yako binafsi? Fikira ya kujiendeleza. Binti yangu anataka kufungua baa. Mtaangamia nyinyi! Maskini wanangu!

**43. MARIAM:** **(Annoyed)** Ma!

**44. ABBAS:** **(Promptly)** Si upotovu, Bibi Sagonda. Tunataka kujikimu maisha yetu. Mambo yamebadilka. Kazi za kibinafsi ndizo zenye faida zaidi siku hizi, na ni vyema kwa maendeleo ya nchi yetu...

**45. SFX : Car approaches and parks.**

**46. SFX : A gate opens and shuts.**

**47. SFX : Steps approach.**

**48. Mrs. SAGONDA:** **(Insistent)** Hapana, wanangu, hapana! Acheni ndoto hizi zenu! Lau tungekuwa matajiri, tungegharamia masomo yenu. Nyote mlitoka shuleni na alama nzuri. **(Sighing deeply)** Ninajua, wanangu, mtaniambia kwamba kuna ukosefu wa kazi na kazi chache zilizopo mishahara yake hairidhishi. Hata hivyo heri nusu ya shari. Tutawasaidia. Abbas, Kossi, wazazi wenu lazima wanajuana na watu. Msijali, tutawatafutia kazi, kazi za kuaminika…

**49. MARIAM:** Lakini Mama….

**50. SFX: PERSON GETS UP FROM A PLASTIC CHAIR**

**51. Mrs. SAGONDA:** (**Gets up. Vehemently**) Tosha. Sitaki kusikiliza tena. Unalotaka halitafanyika hapa; na unamjua babako…

**52. MARIAM:** **(In the same vehement tone)** Lakini tunataka kujisimamia!

**53. KOSSI:** Naam, mama. Tunaka kuwa wabunifu, wagunduzi.

**54. Mr. MASINGA:** (**Silent until now; in an encouraging tone**) Vizuri sana kusikia hiyo, wanangu wapenzi!

**55. Mrs. SAGONDA:** (**Surprised, as is everyone**) Ah ha, binamu! Umekuwa hapo kwa muda gani?

**56. Mr. MASINGA:** Nimekuwa hapa kwa muda wa dakika chache, na nimesikia kila kitu. Mbona hutaki wajiendeleze?

**57. Mrs. SAGONDA:** Hawa watoto watatuangamiza!

**58. Mr. MASINGA:** (**Reassuringly**) Hawawezi! Njoo, kaa chini tena.

**59. SFX : Sound of plastic chairs**

**60. Mr. MASINGA:** Dadangu, ni kweli mambo yamebadilika. Watoto wanasema ukweli.

**61. MARIAM:** (**Very happy**) Ni kweli, sivyo, mjomba?

**62. Mr. MASINGA:** Naam, mwanangu. Ninawaunga mkono. Ningependa kuwahimiza muasisi miradi yenu wenyewe. Kama ulivyosema, ni miradi ya kibinafsi inayonawiri siku hizi. Mataifa yetu yanahitaji hivyo iwapo yanataka

kuendelea. Agatha, dadangu, nitazame. Mimi mwenyewe si leo nimeliinua jina la familia yetu na nchi yetu? Lakini miaka thelathini iliyopita, nilipotaka kujifanyia kazi yangu mwenyewe, kuanzisha kampuni ya LIFE WATER, nyote mlinifikiria mimi kuwa mpumbavu. Kila mtu alinitania. Kila mtu aliniuliza: Utaanzisha je kampuni ya kusafisha maji taka, uyasafishe na kuyatia dawa na uyafunge kwenye mifuko na kuuzia watu …

63. **Mrs. SAGONDA:** (**Disarmed**) Kweli usemavyo…

64. **Mr. MASINGA:** Leo hii, wanangu, maduka yote makubwa katika bara letu yanataka maji kutoka LIFE WATER, ambayo yamekuwa maarufu. Nimefanikiwa si haba!

65. **ABBAS:** Uliwapuuza waliokuwa wakikuvunja moyo?

66. **Mr. MASINGA:** Ndiyo hivyo! Upuuze na ung'ang'ane. Ukitaka kufaulu huna budi kuwa mkakamavu na kuwa na subira. Unapoanzisha biashara yako, si kwamba utafaulu mara moja. Zaidi ya hayo unatakikana kupenda jambo unalofanya. Hakuna jambo lolote kubwa unaloweza kulifanya bila kuwa na mapenzi nalo. Unatakikana kuwa stadi daima kuvumbua, kutafuta mawazo mapya, mawazo mazuri. Wataalamu wanayaita *mawazo ya thamani* …

67. **Mrs. SAGONDA:** (**Worried**) Naam, tutumaini kuwa mambo yatakwenda sawa …

68. **Mr. MASINGA:** Yatakwenda sawa… Msiwe na wasiwasi, jamaa – mkitaka msaada wangu, muibuke na wazo la kipekee.

Mnataka kufanya nini? Katika uwanja gani? Mnalenga watu gani?

**69. KOSSI:** Kwa hivyo, Bwana Masinga, utatusaidia iwapo tutakuwa na wazo la kipekee?

**70. Mr. MASINGA:** Ndio, wanangu! Nitawaunga mkono kwa vyovyote vile....

**71. Mrs. SAGONDA: (Defeated)** HAYA, HAYA. Mwacheni sasa. Henri umekuja kuzungumzia mazishi ya mjomba Bozana? Njoo! Tuingie ndani. Mume wangu ataungana nasi baadaye, amekwenda madukani. **(To her daughter)** Mariam! Ebu ondoa vyombo mezani!

**72. SFX : sound of plates and other things**

**<u>OUTRO</u>**

**Host:**

Hicho kilikuwa kipindi cha kwanza cha mfululizo wa vipindi vyetu vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu kuanzisha biashara, kinachomhusisha mtaalamu wetu Daniel Huba wa Chuo Kikuu cha Inoorero mjini Nairobi. Je wahusika wetu watafanya nini kutimiza ndoto yao? Sikilza kipindi kitakachofuata kwa taarifa zaidi.

Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki, au vipindi vinginevyo vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, tembelea wavuti wetu [www.dw.de/kiswahili](http://www.dw.de/kiswahili)
Kwaheri kwa sasa na usikose kututegea sikio katika kipindi kijacho!

END